

WAMISHIONARI WA KIZUNGU AFRIKA MASHARIKI

Re-arranged and translated by Pastor Stephen Letta

Johannes Ehlers, (aliyezaliwa c.1873)

Johannes Ehlers alikuwa mmoja wa wamishionari wawili wa kwanza wa Waadventista Wasabato nchini Tanzania (iliyokuwa Afrika Mashariki ya Kijerumani wakati huo).

Maisha ya Awali na Ndoa

Johannes (Johann) Ehlers alizaliwa kati ya 1873 na 1876 huko Ujerumani. Ehlers alikuwa mtunza bustani aliyefanikiwa nchini Ujerumani. Alitumia mwaka mmoja katika mafunzo ya misheni katika Shule ya Misheni ya Waadventista huko Friedensau. Mnamo 1902, Ehlers alimuoa Rosa.

Kazi ya Misheni ya Mtangulizi

Ilikuwa mnamo Julai 9-19, 1903, Mkutano wa kwanza wa Kambi ya Wajerumani wa Union Konferensi ya Ujerumani uliofanyika huko Friedensau, ulipofanya maamuzi ya kuingia Afrika Mashariki ya Ujerumani kama eneo jipya la umishionari. Ehlers aliwekwa rasmi kuwa mtangulizi kwa kusudi hili. Ehlers, ambaye alikuwa na umri wa miaka thelathini wakati huo, alitawazwa kama mzee wa kanisa kwa kusudi hili pia. Ehlers alijiunga na Abraham C. Enns. Hawa waliunda timu na kuagizwa wafanye kama wapelelezi ili “kuipeleleza nchi na kufahamu fursa za kimishionari zinazopatikana.”

Mnamo Oktoba 22, 1903, Ehlers na Enns, (muuguzi aliyefunzwa), walipanda manowari iliyokuwa ikielekea Afrika Mashariki, wakawasili Dar-es-Salaam, kusini mwa kisiwa cha Zanzibar, Novemba 12, 1903. Ehlers alikuwa amemwacha mke wake, Rosa, huku Enns akimwacha mchumba wake huko Ujerumani. Alipofika Dar es Salaam, Gavana wa Tanganyika aliwapokea na kuwaalika Ehlers na Enns kwa chakula cha jioni. Baada ya chakula walijadili utume wao na Mkuu wa Mkoa. Baada ya mazungumzo kadhaa na Gavana, wamishionari walianza umishionari wao kaskazini-magharibi mwa Tanganyika, katika Pare Kaskazini, iliyoko Same – Kilimanjaro.

Gavana huyo pia aliwapa barua ya kuwatambulisha kwa vituo vyote vya kijeshi iliyoidhinisha kwamba wamishionari “wapewe msaada wowote ambao wangehitaji, ama kwa njia ya shauri katika kuchagua kituo, au kwa waongozaji na wabebaji, au kwa askari wa kuwalinda ikibidi.” Kufikia mwisho wa mwezi kituo cha misheni kilikuwa kimepatikana miongoni mwa watu katika Milima ya Pare. Majengo yalijengwa, na kituo cha misheni kilipewa jina la Friedenstal yaani bonde la amani.

Kati ya Februari na Machi 1904, Rosa Ehlers, ambaye aliazimia kuungana na mume wake kuendeleza kazi ya umishionari, alisafiri pamoja na wamishionari wengine wanne: Ludwig R. Conradi, Christoph Wunderlich, August Langholf na mke wake Frieda Breitling kutoka Hamburg, Ujerumani hadi Tanganyika. Conradi, kiongozi wa Waadventista huko Ulaya wakati huo, alitaka kujionea mambo yalivyo kwenye eneo jipya la Tanganyika walikoanzisha kazi. Ziara ya Conradi lazima iwe iliwezesha

WAMISHIONARI WA KIZUNGU AFRIKA MASHARIKI

Re-arranged and translated by Pastor Stephen Letta

mipango ya ujenzi wa shule na ununuzi wa punda wawili kusaidia wamishionari na kuimarisha harakati ndani ya jamii ya Wapare.

Nchini Tanganyika, familia ya Ehlers ilibarikiwa kupata watoto wawili. Wakati huo huo, Ehlers mwenyewe alikuwa amejifunza lugha ya Kisambaa na Kipare ili kumsaidia kuwafikia Wapare. Alijishughulisha na mihadhara ya watu wote, uinjilisti wa vitabu na kuendesha madarasa ya Biblia majumbani ili kueneza injili. Mnamo Februari 1906, Ehlers aliugua katika eneo la kimishionari.

Baadaye mwaka huo huo, familia ya Ehlers ilirudi Ujerumani kwa sababu ya afya mbaya ya Johannes. Waliishi Ellerau karibu na Hamburg, ambapo Rosa, mke wake alimtunza. Hata hivyo, kabla ya kurudi kwao, ilionekana kuwa Rosa alikuwa ameambukizwa malaria. Baada ya kujisikia baridi, Rosa Ehlers aliugua malaria. Alikufa mnamo Februari 13, 1907, akimwacha mume wake dhaifu na watoto wawili wadogo.

Hakuna mengi yanayopatikana kuhusu Ehlers baada ya mkewe kufariki. Ingawa rekodi ya hali halisi inaonekana kuwa kimya kuhusu hatima ya Ehlers kwa ujumla, ila kuna uwezekano kuwa alikufa wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia, au alikufa kwa mafua, au alihamia nchi nyingine.

Mchango Aliotuachia

Urithi wa Johannes Ehlers unafungamanishwa kwa karibu na maingilio ya Waadventista Wasabato katika iliyokuwa Afrika Mashariki ya Kijerumani. Jitihada za Ehlers kama mmishionari mtangulizi zilikuwa muhimu katika kuweka msingi uliochochea ukuaji wa Kanisa la SDA katika nchi ambayo inajivunia mamia kwa maelfu ya waumini wa Kiadventista – Tanzania ya leo.